JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA PANGANI

**Kumb.Na.HWP/T.40/5/VOL.11/6** **30.10.2024**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MKATABA ZA MADEREVA WA TREKTA

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani anawatangazia watanzania wote wenye sifa ya kujaza nafasi za kazi za mkataba wa udereva wa trekta.

**DEREVA WA TREKTA – NAFASI 4**

**2. MAJUKUMU YA KAZI**

i. Kukagua trekta kabla na baada ya kulima ili kubaini hali ya usalama wa trekta;
ii. Kulima mashamba ya wakulima kwa ajili ya kupanda kulingana na maelekezo yatakayotolewa na wasimamizi
iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya trekta;
iv. Kufanya usafi wa trekta na
v. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

S.L.P 89 Pangani, Simu 027 2977485, Barua Pepe: ded@panganidc.go.tz, Tovuti: www.panganidc.go.tz

CamScanner

### 3. SIFA ZA MWOMBAJI

i. Awe na leseni ya udereva Daraja G ya uendeshaji matrekta ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja
ii. Awe na uzoefu wa shughuli za kulima kwa kutumia trekta usiopungua mwaka mmoja

### 4. MSHAHARA

Malipo yatafanyika kwa ekari zitakazolimwa

### MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka18 na usiozidi miaka 45
ii. Awe na tabia njema na maadili
iii. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ya udereva ni tarehe 08 Novemba, 2024.
iv. MUHIMU: Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa: - **Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, S. L. P. 89, PANGANI.**

**Charles Edward Fussi**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**PANGANI**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA (W)
PANGANI

S.L.P 89 Pangani, Simu 027 2977485, Barua Pepe: ded@panganidc.go.tz, Tovuti: www.panganidc.go.tz

CamScanner